**HOTUBA YA BALOZI BRIG. GEN. WILBERT A. IBUGE, KATIBU MKUU WA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI WAKATI WA UFUNGUZI WA MKUTANO WA SITA (6) WA TUME YA PAMOJA YA KUDUMU YA USHIRIKIANO KATI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NA JAMHURI YA BURUNDI KATIKA NGAZI YA MAKATIBU WAKUU**

**TAREHE 03 MACHI, 2021, KIGOMA**

***Mheshimiwa Isidore Ntirampeba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimaendeleo wa Jamhuri ya Burundi na Mwenyekiti Mwenza wa Kamati ya Makatibu Wakuu ya Mkutano huu;***

***Waheshimiwa Makatibu Wakuu wenzangu Mliopo Hapa;***

***Mheshimiwa Rashid Mchatta, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma;***

***Mheshimiwa Dkt. Jilly Maleko, Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Jamhuri ya Burundi;***

***Mheshimiwa Cyriaque Kabura, Konseli Mkuu wa Jamhuri ya Burundi hapa Kigoma ambaye pia anamwakilisha Balozi wa Jamhuri ya Burundi nchini Tanzania;***

***Watumishi wa Serikali wa pande zote mbili mliopo hapa;***

***Mabibi na Mabwana;***

**Habari za asubuhi!**

**MWAKEYEE au AMAHORO MWESI *(Mojawapo)***

**MLIMOO**

## SALAMU ZA UTANGULIZI NA UKARIBISHO

Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuturuzuku uhai na kutuwezesha kukutana siku ya leo hapa Kigoma kwa ajili ya shughuli

hii adhimu inayolenga kuimarisha zaidi uhusiano na ushirikiano uliopo kati ya nchi zetu za Tanzania na Burundi.

Kwa namna ya kipekee napenda kuchukua fursa hii kukukaribisha tena **Mheshimiwa Isidore Ntirampeba**, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimaendeleo wa Jamhuri ya Burundi pamoja na Ujumbe wako. Karibuni sana Tanzania, karibuni Kigoma. Jisikieni huru kwani hapa ni nyumbani kwenu pia! **Huku Kigoma tunasema tulashashe Mhila Mkigoma.**

## DHUMUNI LA MKUTANO

***Ndugu Viongozi Wenzangu na Wajumbe Mkutano huu;***

Mtakumbuka kuwa, tarehe 19 Septemba, 2020, Wakuu wa Nchi zetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Jenerali Evaristé Ndayishimiye, Rais wa Jamhuri wa Burundi walikutana hapa Kigoma, Mhe. Ndayimishiye alipofanya ziara ya kikazi kwa mwaliko wa mwenyeji wake Mheshimiwa Dkt. Magufuli.

Wakati wa ziara hiyo, Viongozi wetu Wakuu hao walikubaliana masuala kadhaa yenye lengo la kuimarisha zaidi ushirikiano tulionao kwa ustawi wa nchi zetu na watu wake. Moja ya maazimio yao lilikuwa ni suala la Mkutano wa Tume ya Kudumu ya Pamoja kati ya Tanzania na Burundi (JPC) kufanyika kabla ya mwezi Aprili, 2021. Hivyo, tunafanya Mkutano huu kwa lengo la kutekeleza maagizo na makubaliano hayo ya Wakuu wa Nchi zetu. Pia, tunakutana kujadili utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa kwenye Mkutano wa JPC ya mwisho uliofanyika mwaka 2006. Vilevile, tunakutana ili kujadili fursa nyingine lukuki zilizopo za ushirikiano kati ya nchi zetu hizi mbili rafiki.

***Ndugu Wajumbe;***
***Mabibi na Mabwana;***

Kufuatia maelekezo husika ya viongozi wetu Wakuu, Tanzania ilianza utekelezaji wa maagizo hayo mapema kwa namna inavyouthamini uhusiano wake na Burundi. Kwa mfano, kuanzia tarehe 26 hadi 30 Septemba, 2020, Wizara pamoja wadau wengine wa kisekta ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya Kikanda ya miundombinu inayotekelezwa na Serikali za nchi zetu mbili chini ya uratibu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kuhakikisha kwamba miundombinu hiyo inatumika ipasavyo katika kuimarisha biashara kati ya nchi hizi na hivyo kuchangia kwenye jitihada za maendeleo.

Pamoja na masuala mengine kwenye ziara hiyo, tulikagua mradi wa Ujenzi wa **Barabara ya Kabingo – Kasulu – Manyovu (km 260.13)** yenye thamani ya dola za Marekani milioni 256. Mradi huu unahusisha pia **Ujenzi wa Kituo cha Huduma kwa Pamoja Mpakani (OSBP)** cha **Manyovu/Mugina**. Kufuatia ziara hiyo, **Hati ya Makubaliano (MoU) ya kuratibu shughuli za Ujenzi wa Barabara ya Kabingo – Kasulu – Manyovu (260km) / Rumonge – Gitaza (45km)** ilisainiwa **tarehe 02 Novemba, 2020.** Aidha, makabidhiano ya eneo kitakapojengwa Kituo cha Huduma kwa Pamoja Mpakani (OSBP) cha **Manyovu/Mugina** yalikamilika kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

***Ndugu Wajumbe;***
***Mabibi na Mabwana;***

Shughuli nyingine za kuimarisha ushirikiano kati ya nchi zetu mbili zilizofanyika kabla ya Mkutano huu wa JPC ni pamoja na **mkutano wa pamoja wa Sekta ya madini uliofanyika mwezi Januari 2021**, hapa mkoani Kigoma ambapo wajumbe wa pande zote mbili walijadiliana namna bora ya kushirikiana katika sekta hiyo. Hivyo, Mkutano

huu wa sita (6) cha JPC ni fursa muhimu sana katika kujadili maeneo mengine ya ushirikiano kwa faida ya nchi zetu.

## MKUTANO WA SITA WA JPC YA TANZANIA NA BURUNDI

***Ndugu Wajumbe;***
***Mabibi na Mabwana;***

Tunapokutana kwa ajili ya Mkutano huu wa JPC ni muhimu kutambua kuwa nchi zetu zimeendelea kuwa na uhusiano na ushirikiano mzuri kwa muda mrefu. Tanzania na Burundi ni majirani, ndugu wa karibu na marafiki wa muda wote. Ukaribu wetu unadhihirishwa na namna ambavyo tumeendelea kushirikiana katika masuala mbalimbali ikiwemo masuala ya ulinzi na usalama; biashara, uwekezaji, maliasili na utalii, uvuvi, kilimo, nishati, madini, elimu, afya, utamaduni, masuala mengine ya kijamii kama vile shughuli za kiutamaduni na michezo.

***Ndugu Wajumbe,***

Nchi hizi pia zimeendelea kushirikiana katika masuala ya Kikanda na Kimataifa kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR), Umoja wa Afrika (AU) na Umoja wa Mataifa (UN). Nitumie fursa hii kuuhakikishia tena ujumbe wa Burundi kwamba Tanzania itaendelea kuunga mkono ombi lake la kuwa nchi Mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Aidha, tutaendelea kuisemea Burundi katika majukwaa ya kimataifa ili iondolewe vikwazo vyote vya kiuchumi ilivyowekewa. Ni kwa muktadha huu pia tunatoa pongezi kwa Burundi kwa hatua mbalimbali inazoendelea kuzichukua katika kuleta maendeleo ya wananchi wake, kuimarisha hali ya usalama na kuimarisha uhusiano na jumuiya ya kimataifa. Hatua hizi, pamoja na masuala mengine, zimewezesha Taifa hilo

kuondolewa kwenye ajenda ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, suala linalostahili kupongezwa.

***Ndugu Wajumbe;***
***Mabibi na Mabwana;***

Mtakubaliana na mimi kuwa mafanikio ya mkutano huu yanategemea zaidi jitihada zetu za pamoja sisi Watendaji katika kutekeleza masuala tutakayokubaliana. Hivyo, nitoe wito kwetu sote kujadili kwa uhalisia na kufikia makubaliano yanayotekelezeka. Pia tuwe tayari kusimamia na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa makubaliano hayo. Ni muhimu pia tuweke utaratibu wa kufanya mapitio ya utekelezaji wa masuala tunayokubaliana angalau mara moja kwa mwaka, na niwahakikishie kwamba kwa upande wa Tanzania, tutakuwa tunafanya mapitio ya mara kwa mara ya makubaliano yote tuliyofikia. Kwa kufanya hivyo, Mkutano huu wa JPC utatimiza matarajio ya Viongozi wetu Wakuu pamoja na wananchi wa Mataifa yetu.

***Ndugu Wajumbe;***
***Mabibi na Mabwana;***

Tanzania ina matumaini makubwa kwamba Mkutano huu utakuwa wa mafanikio kwa ustawi wa nchi zetu na watu wake. Hivyo, naomba kuwatakia wote pamoja na mimi mweyewe, Mkutano mwema na majadiliano yenye tija. **Aidha, ninayo heshima sasa ya kutangaza kuwa Mkutano huu wa Sita (6) wa Tume ya Pamoja ya Kudumu kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Burundi umefunguliwa rasmi.**

**Karibuni sana Tanzania!**
**Kaze Muri Tanzania!**
**Bienvenue en Tanzanie!**

**Asanteni sana!**

**Murakoze Chanee!**

**Merci Beaucoup!**